## *Hatua moja isiyofaa kwa mtu mmoja mzuri yaweza kuleta shida moja kubwa.*

Katika mwaka wa 1912, meli ilyokuwa kubwa zaidi duniani ya kuvinjari, ilinoa nanga kule Liverpool, Uingereza na ikaanza safari yake ya kwanza. Ilikuwa inaelekea Marekani na iliitwa Titanic. Titanic, ilikuwa imeundwa na watu wenye ustadi mwingi wa ujenzi na ilikuwa na nahodha mwenye ujuzi mwingi. Ingawa kulikuwa kumetolewa ilani ya kuwa jiwe kubwa barafu lilikuwa limeonekana na wakaonywa, amri ya kuendelea kwenye maji ya barafu kwa kasi isiyo ya hekima ilitolewa. Kwa mda wa masaa kidogo, uamuzi mmoja wa kutojali uliofanywa na na mtu mmoja mzuri, ulisababisha shida moja kubwa. Meli iligonga jiwe la barafu na yaliyofuatia ni historia.

Mungu ameyaunda maisha yetu na kuyaweka kwenye ukingo. maamuzi yanahitajika kila siku. Ni muhimu kwamba tuelekeze maisha yetu kupitia kwa Neno la Mungu ili tuweze kuendelea safari yetu, bila kusababisha shida kwetu wenyewe ama kwa wengine kwa maaamuzi ya kutojali.

*Ombi la leo*
Nisaidie Bwana, kuchukua wakati na kufikiria kuhusu matendo yangu na amuzi za maisha yangu. Dhihirisha Neno Lako kwangu na wacha kila wakati iwe ndiyo desturi yangu kutafuta ushauri Wako kuhusu amuzi ninazozifanya.

*Maandiko ya leo:*
Zaburi 119:105; Neno Lako ni taa ya miguu yangu  na nuru ya njia yangu

Zaburi 37:23; hatua za mtu mwenye haki zinaelekezwa na Bwana, na Yeye hufurahishwa na mapito yake.

## *Huenda ikawa uko sahihi na wengine wakawa wamenoa, hata hivyo, kama wale Mungu ameweka maishani mwako, wanaokupenda na wanamtumikia Mungu pamoja na wewe wana maswali, kuna sababu ya kujihadhari.*

Nyakati zingine maishani twaweza kuwa na tamaa ama tuwe na hangaiko la kufanya amuzi tunazoona kwa uwazi kuwa ni za usawa

kwetu. Tunapofanya amuzi, hasa amuzi zinazobadilisha maisha yetu, twafaa kujichunguza kwa kina na kutafuta ushauri kutoka kwa Neno la Mungu, na watu ambao Amewaweka kwa maisha yetu.

Wakati mwingi uamuzi wetu waweza kuwa hauoni vizuri na hauoni mbali ilhali wengine waweza kuona matokeo ambayo hatukuwa tumebashiri. Hakuna yeyote anayeweza kuwa Roho wako Mtakatifu, hata hivyo huwezi puuza ushauri mzuri kutoka kwa watu wanaojali. Kama unaogopa kusikia kile watu wengine ndani ya maisha yako wanataka kusema kuhusu uamuzi huo wako…jiulize ni kwa nini.

*Ombi la leo*
Mungu, ahsante kwa Uongozi Wako wa kiungu na mwelekezo na pia kwa sababu ya husiano maishani mwangu. Nipe hekima na sikio la kusikiza kukusikia Wewe na kufuata mpango Wako kuhusu maisha yangu.

*Maandiko ya leo*
Mithali 11:14; pasipo mashauri taifa huanguka; bali kwa wingi wa ushauri huja wokovu.
Kutoka 18:19;sikiza sasa neno langu, nitakupa ushauri, na Mungu na awe pamoja nawe; uwe wewe kwa ajili ya watu mbele za Mungu, nawe umletee Mungu maneno yao. Nawe utawafundisha zile amri na sheria, nawe utawaonyesha njia ambayo wanapaswa kuiendea, na kazi ambayo wanapaswa kuifanya.

## *Mambo makuu yanayofanywa kwa Mungu na mambo yakifanywa makuu kwa Mungu, kulingana na historia, yanalazimu dhabihu.*

Mungu hakumtoa mwanaye wa ziada ila wa kipekee kwa sababu ya dhambi zetu. Mungu hakumtoa mwanaYe wa kipekee peke yake lakini Mariamu alimtoa mzaliwa wake wa kwanza. Inagharimu mbingu na dunia kuyafanya mambo makuu kwa Mungu na kufanyia Mungu mambo kwa njia kubwa. Kila kusudi na kila mwelekeo hugharimu kulipa gharama na kujitwalia. Huyo mtu aweza kuwa wewe.

Mambo makuu yakifanywa kwa Mungu na mambo yakifanywa makuu kwa Mungu kulingana na historia, hugharimu dhabihu. Usiwache kuchangia kwako ama ukose kufuatilila shani za kifalme kwa vile zinagharimu muda zaidi, nguvu, na jitihada kuliko ulivyowazia hapo awali. Kama hautamaliza jukumu ulilonalo…ni nani atakayemaliza? Usimuwache Mungu.

*Ombi la leo*

Baba, nipe ujasiri leo kuhesabu gharama na kulipa bei ili nifanye mambo makuu kwa ajili Yako. Fanya upya imani yangu ninaposoma Neno, nikikumbuka mitume wa zamani, dhabihu walioitoa, lakini zaidi ya yote, malipo yaliyofuatia uaminifu wao! Nataka kuwa wa faida Kwako na ufalme Wako.

*Maandiko ya leo*

Waebrania 10:38-39Lakini mtu wangu aliye mwadilifu ataamini na kuishi; walakini akirudi nyuma, mimi sitapendezwa naye." Basi, sisi hatumo miongoni mwa wale wanaorudi nyuma na kupotea, ila sisi tunaamini na tunaokolewa.

Mathayo Mtakatifu 19:21-22; Yesu akamwambia, "Kama unapenda kuwa mkamilifu, nenda ukauze mali yako uwape maskini hiyo fedha, nawe utakuwa na hazina mbinguni, kisha njoo unifuate." Huyo kijana aliposikia hayo, alienda zake akiwa mwenye huzuni, maana alikuwa na mali nyingi.

## *Wakati mwingine dhabihu kubwa tunayoweza kumtolea Mungu Ni swali tulilinalo ambalo hatuna jawabu.*

Hatari, kuumizwa rohoni, kufanya makosa, kifo ama usaliti… kuna mambo mengi maishani hasiyo na jawabu za kulidhisha. Labda fursa yetu kuu ya kuwa na imani ni nyakati ambapo kunakaa kama hakuna sababu ilhali tunajua Mungu alo kwa usukani.

Ayubu alitafuta jawabu alipokuwa na mateso. Aliumia kukosa pesa na kupoteza kwa kibinafsi. Hatimaye, Mungu aliweka wazi kuwa ni Yeye pekee ambaye ni Mkuu. Ingawa aweza kutupea jawabu, sio lazima atuelezee ni kwa nini. Huyu Mungu wa upendo na kutjali tunayemtumikia, ana mtazamo wa kiumilele ambao hatuwezi tukawazia na wala kubishania. Muamini Mungu hata wakati maisha inaonekana kama hayana mwelekeo.

*Ombi la leo*

Mungu, nisaidie Leo ni kuamini kwa kabisa. Bila kuangalia hali zangu, majaribu, ama mahatari ya dunia hii, nachagua kuamini kwamba unanipenda, Hautaniacha wala kunisahau Na kwamba una mpango mzuri kuhusu siku zangu za usoni. Imani yangu iko Kwako pekee.

*Maandiko ya leo*

Ayubu 13:15; tazama, utaniua; sina tumaini. Ila hata hivyo, nitaidhibitisha njia yangu mbele yake.

Zaburi 62:8; enyi watu; mtumainieni siku zote. Ifunueni mioyo yenu mbele zake, Mungu ndiye kimbilio letu.

## ***Mawazo yetu huumba dunia tunayoishi ndani yake na kudhibitisha jinsi tunavyoishi duniani.***

Tunachofikiria kuhusu vile tulivyo na kile tunachoweza kutenda labda yaweza kutuwekea kiwango ama kuondoa viwango maishani mwetu. Kila mmoja wetu huumba dunia tunayoishi ndani yake nakuijaza na mawazo yetu. Huenda ikawa hii ni sababu moja kwa nini Bibilia ina mengi ya kusema kuhusu maisha ya fikira zetu. Kwa hakika, Mithali 23:7 inasema, “ maana aonavyo nafsini mwake, ndivyo alivyo…”

Unawazia nini kujihusu mwenyewe? Umeumba dunia gani? Unamtazamo upi na unaishi maisha vipi? Wewe ni mshindi ama wewe ni mwadhiriwa? Unaajiwazia kushinda ama kushindwa? Unafikiria Mungu anakupenda na anampango juu ya maisha yako ama unahisi amekusahau? Vita vya wewe ni nani na vile utakavyoishi huanza na kuishia ndani ya mawazo yako. Jaza mawazo yako na Neno la Mungu na uwache achukue usukani wa fikira zako.

*Ombi la leo*

Baba, nachagua kujaza mawazo yangu na Neno Lako na niishi maisha yaliyo na mtazamo wa mbinguni. Natupilia mbali mawazo na fikira zangu na wengine ambazo haziambatani na mapenzi Yako.

*Maandiko ya leo*

Warumi 12:2; Msiige mitindo ya ulimwengu huu, bali Mungu afanye mabadiliko ndani yenu kwa kuzigeuza fikira zenu. Hapo ndipo mtakapoweza kuyajua mapenzi ya Mungu, kutambua jambo lililo jema, linalompendeza na kamilifu.

2 Wakorintho 10:4-5; Maana, silaha tunazotumia katika vita vyetu si silaha za kidunia, ila ni nguvu za Mungu zenye kuharibu ngome zote. Tunaharibu hoja zote za uongo, na kubomoa kila kizuizi cha majivuno kilichowekwa kuipinga elimu ya Mungu; tunaziteka fikira zote na kuzifanya zimtii Kristo.

Wafilipi 4:8; hatimaye, ndugu zangu, mambo yo yote yaliyo ya kweli, yo yote yaliyo ya staha, yo yote yaliyo ya haki, yo yote yaliyo safi, yo yote yenye kupendeza, yo yote yenye sifa njema; ukuwapo wema wo wote, ikiwapo sifa nzuri yo yote, yatafakarini hayo.

## ***Mungu hatuombi ruhusa kabla ya kuharibu mipango yetu.***

Maisha ni safari, andiko ambalo ni Mungu pekee anayeweza kuandika na shani iliyopita ulimwengu huu. Mungu ndiye mwanzilishi na mkamilishi wa maisha yetu na anaona mwisho kutokana na mwanzo. Maisha yetu ni mpango wa Mungu na anapanga mambo yote kutendeka kulingana na mapenzi na makusudi Yake. Twaweza kuwazia mapito yetu lakini ni Bwana anayeelekeza hatua zetu.

Kinacho onekana kama kwamba chakustaajabisha ni mpango kwa Mungu na Mungu sio lazima atuombe ruhusa kabla aiharibu mipango yetu. Maisha hugharimu amuzi zetu na Mungu hugharimu tuweke uamuzi hizo kwa mikono Yake na kumuaminia abadilishe kinachohitaji kubadilishwa na kutimiza mapenzi Yake, sio yetu.

*Ombi la leo*

Baba, niongoze leo na unisadie kufuate njia ambayo umenitengenezea. Nisaidie kutambua ya kwamba labda niko ndani ya mapenzi Yako kuliko vile ninavyotambua. Nataka kukufuata na mpango Wako kwa kuwa hatima Yako ni bora.

*Maandiko ya leo*

Mithali 16:9; moyo wa mtu huifikiri njia yake; mbali Bwana huziongoza hatua zake

Isaya 46:10; nitangazaye mwisho tangu mwanzo, na tangu zamani za kale mambo yasiyo tendeka bado; nikisema, shauri langu litasimama, nami nitatenda mapenzi yangu yote.

Muhubiri 3:11; kila kitu amekifanya kizuri kwa wakati wake; tena ameiweka hiyo milele ndani ya mioyo yao; ila kwa jinsi mwanadamu asivyoweza kuivumbua kazi ya Mungu anayoifanya, tangu mwanzo hata mwisho.

## *Jeshi la Mungu halijakusudiwa kuhifadhi mahali ambapo Mungu amekuwepo na kile Mungu ametenda, ila kufuata mahali ambapo Mungu anataka kuenda na ambacho Mungu anataka kutenda.*

Walioitwa katika jeshi la Mungu ni lazima waelewe ya kwamba lazima tuhusika na kuendeleza injili hii hadi dunia nzima isikie.hatuwezi kutoshelezwa na kile Mungu ametenda tayari lakini lazima tuendelee mbele kutimiza anachotaka kutenda. Kanisa, jeshi la Mungu, sio hifadhi ya barafu ila ni hifadhi ya joto.

Watenda dhambi wanazaliwa kila siku na vizazi hupitia dunia hii wakiwa wameishi fursa yao ya kusikia Neno Njema na kumfanya Yesu kuwa Bwana wao.haitoshi ya kwamba kizazi kimoja kimesikia… kila kizazi lazima kisikie. Na kwa hivyo lazima tuendelee mbele tukukesha tukiwa tumeamua kuafikia mapenzi ya Mungu tukiwa bado tuna wakati.

*Ombi la leo*

Baba, nipe neema na msukumo wa kutenda kazi katika mashamba Yako mradi niko na uhai. Nisaidie kufunza wengine umuhimu wa kuendelea mbele katika Mwito Mkuu hadi dunia nzima isikie.

*Maandiko ya leo*

Yoshua 1:2; Musa mtumishi wangu amekufa; haya basi, ondoka, vuka mto huu wa Yordani; wewe na watu hawa wote, mkaende hata nchi niwapayo wana wa Isiraeli.

Wafilipi 3:13; ndugu, sijidhanii nafsi yangu kwamba nimekwisha kushika nini; ila natenda neno moja tu; nikiyasahau yaliyo nyuma, nikiyachuchumilia yaliyo mbele;

## *Siku moja amuzi unazofanya maishani, zitafanyika ushuhuda wako wa mwisho.*

Hadithi ya maisha yako ni kama kitabu kinachofululiza kuandika, kurasa hadi nyingine kuhusu kila uamuzi na kitendo cha maisha. Kwa hakika hata fikira zako zinanakiliwa kwa marudio ya mwisho ya umilele. Maisha yetu ya milele yamelindwa na uamuzi unaofanya kumkumbali

Yesu Kristo kama Bwana na mwokozi. Ni kupitia damu Yake na damu Yake pekee tumeokolewa.

Hata hivyo, kila mtu atapokea dhawabu ya umilele kupita wokovu kulingana na amuzi na kazi zilizotendwa katika maisha haya. Kwa wakati wowote ule tuko huru kufunga sura maishani na kuanza kuandika hadithi mpya ambayo siku moja itasimuliwa kama ushuhuda wetu wa mwisho. Daudi alitenda; Petero alitenda; Zakayo alitenda; Ruthu alitenda; Rahabu alitenda; Paulo alitenda… na pia wewe waweza!

*Ombi la leo*

Baba, amuzi ninazofanya leo zitaadhiri siku zangu za usoni kwa kuwa muda mfupi nilionao duniani ndio fursa pekee nitayopata kuadhiri umilele, tafadhali nisaidie kufanya amuzi zenye hekima. Nisaidie kuwa na mtazamo wa kifalme ninapoweka kipa umbele za maisha yangu. Kwa neema Yako naanza leo.

*Maandiko ya leo*

Ufunuo wa Yohana 20:12; Kisha nikawaona wafu wakubwa na wadogo, wamesimama mbele ya kiti cha enzi, na vitabu vikafunguliwa. Halafu kitabu kingine, yaani kitabu cha uzima, kikafunguliwa pia. Wafu wakahukumiwa kadiri ya matendo yao, kama ilivyoandikwa ndani ya vitabu hivyo .

2 Wakorintho 5:10; Maana sote ni lazima tusimame mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo, ili kila mmoja apokee anayostahili kwa matendo aliyoyafanya wakati alipokuwa anaishi duniani, mema au mabaya.

## ***Maisha ni zaidi ya mlango ulio wazi***

Fursa hupatikana maishani na hututunukia mielekeo mingi ambayo twaweza chagua kwa urahisi. Hata hivyo sababu tu kuwa tuna fursa ya kuchukua kazi mjini tofauti ama kununua kitu kipya haimaanishi ni mapenzi ya Mungu. Pia sio mara wakati huwa mapenzi ya Mungu kupitia mlango wa maisha kwa sababu tu uko wazi na unakualika wewe. Maisha ni zaidi ya mlango ulio wazi.

Amuzi zetu zafaa kuwa na msingi wa uongozi unao kubaliana na Neno la Mungu, Roho wa Mungu, na ushauri wa marafiki, jamii na wengine ambao Mungu amewaweka maishani mwetu. Hakikisha hauishi maisha ukikubali kila mlango ulio wazi kama mapenzi ya kiungu ya Mungu.

*Ombi la leo*

Mpenzi Mungu, nifunze kujua Neno Lako, kuongozwa na Roho Wako na kupokea sauti ya washauri wa kiungu ili nipatikane nikiyafanya mapenzi Yako na sio yangu binafsi. Katika jina la Yesu, Amina.

*Maandiko ya leo*

Wafilipi 4:7; na amani ya Mungu ipitao ufahamu wa mwanadamu, ilinde nafsi zenu na mawazo katika jina la Kristo Yesu.

Wakolosai 3:15; Nayo amani ya Kristo itawale mioyoni mwenu; maana kwa ajili hiyo ninyi mmeitwa katika mwili huo mmoja. Tena muwe na shukrani!

Warumi 8:14; Wote wanaoongozwa na Roho wa MUngu ni watoto wa Mungu.

## ***Sio kile ulicho nacho...ni utakachofanya na kile ulicho nacho kinacholeta utofauti.***

Nimesikia inasemekana kwamba watu hawajali kile ulicho nacho hadi wajue unajali. Ni vivyo hivyo wakati watu wanaangalia ulicho nacho. Hadi ukubali kufanya jambo ambalo kwa hakika litawafaidi wengine na kile ulicho nacho, kile uko nacho hakitaleta utofauti wa kudumu kwa mtu yeyote.

Mungu alimwambia Anrahamu kuwa angembariki na angemfanya yeye pia kuwa wa baraka. Haingejalisha sana kama Abrahamu angekubaliwa na abarikiwe naye Mungu na aweke hizi baraka ziwe za kibinafsi. Badala yake alimchuka Isaka kwa imani, akamtoloa Mungu kama ishara ya kile Mungu angefanya siku moja na Yesu, mwana Wake. Kile Abrahamu alitenda na kile Mungu alimpea yeye na kile tunafanya na kile Anachotupea ndicho kina leta utofauti.

*Ombi la leo*

Baba, kama yule kijana mdogo aliyekuwa na mkate na samaki, hata mimi nataka kuchukua kile nilicho nacho, nikitoe kwako na nilete utofauti. Nisaidie nisiwe mchoyo na nibariki wengine na baraka unazonipea mimi.

*Maandiko ya leo*

Mwanzo 12:14; na Abrahamu akaita jina la mahali pale, Mungu-atatwalia; na inasemwa hivyo hata siku ya leo, “ katika mlima wa Bwana itatwaliwa.”

Yohana 6:11; Yesu akaitwaa ile mikate, akamshukuru Mungu, akawagawia watu waliokuwa wameketi; akafanya vivyo hivyo na wale samaki, kila mtu akapata kadiri alivyotaka.

## ***Mungu anampango, atafaulu na una fursa ya kushiriki***

Mara tena, Bibilia hutuambia kwamba Mungu anajua mwisho kutokana na mwanzo. Yeye ni Alpha na Omega, wa kwanza na wa mwisho, mwanzilishi na mkamilishaji wa imani yetu. Ni Mungu pekee, anayejua mambo yote ambayo yamekuwa, yaliyopo na yatakayokuwa na anayeweza kuanzilisha maisha, kusimamia hali, kuumba hali na kutimiliza ndoto  anapofanya mambo yote pamoja kutimiliza mapenzi Yake.

Sio kwa wahusika wa kale wa Bibilia, ama mtu mmoja anayeishi leo ahitajika kuogopa siku zake za usoni ama matokeo yake ya mwisho kama tu wataweka imani yao kwa Mungu na mwanaye Yesu Kristo, Masii. Mungu ana mpango. Atafaulu na uko na nafasi ya kuhusika.

*Ombi la leo*

Baba, ahsante kwa kunipenda mimi! Hakuwacha chochote kikuzuie kunipea uzima wa milele, na ninashukurani sana kwa ajili ya hayo! Tafadhali usiwahi kuniwacha nikuzuie kupea wengine zawadi kama hiyo. Nataka kile unataka , Bwana- kwa watu wote wakujue Wewe. Tafadhali Bwana, nionyeshe jinsi unatumia  hata nyakati ngumu maishani mwangu kuwaleta wengine Kwako.

*Maandiko ya leo*

Zaburi 46:10; kuwa kimya na ujue Mimi ni Mungu! Nitaheshimiwa na kila taifa. Nitaheshimika dunia nzima.

1 Wakorinitho 15:57; Lakini tumshukuru Mungu anayetupatia ushindi kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo.

1 Wakorinitho 2:14; Mtu wa kidunia hapokei mambo ya Roho wa Mungu. Kwake mtu huyo mambo hayo ni upumbavu mtupu; yanapita akili yake; maana yanaweza tu kutambuliwa kwa msaada wa Roho.

## *Shida ya Dola Ni kwamba hutumika mara moja Tu.*

Neno la Mungu hutunenea kuhusu fedha zetu za kibinafsi. Kwa hakika, Yesu alikuwa na mengi ya kusema kuhusu pesa kuliko alivyosema kuhusu mbingu na jehanamu, kama zimekusanyishwa. Ni mpango wa Mungu iwe na vitu. Hata hivyo, hataki vitu vikupate wewe.Mungu akitubariki sisi, hufanyika wangojezi wa baraka hizo na kwa hivyo tunatarajiwa kusimamia pesa zetu kwa hekima ya uungu na kanuni ya Kibibilia.

Mara nyingi, sababu hauwezi kununua unachotaka ni kwa vile ulinunua kile ulitaka. Ni muhimu tusimamie pesa zetu tukitilia maanani makusudi ya Mungu na sio tu yetu binafsi. Shida ya dola hata wakati tumepewa na Mungu, ni kwamba inatumika mara moja. Tumia pesa zako kwa busara.

*Ombi la leo*

Baba, ahsante kwa kunitwalia mahitaji yangu yote! Ninajua kila nilicho nacho ni chako wewe. Tafadhali nionyeshe ni wapi naweza kufanya amuzi za busara ni wapi nitatumia dola yangu. Najua utanishughulikia na ubariki utiifu wangu. Tafadhali chukua ninachopeana na utumie na ufanye utofauti wa umilele.

*Maandiko ya leo*

Mathayo Mtakatifu 6:19-20; "Msijiwekee hazina hapa duniani ambako nondo na kutu huharibu, na wezi huingia na kuiba. Jiwekeeni hazina mbinguni ambako nondo na kutu hawawezi kuiharibu, wala wezi hawaingii wakaiba.

Waefeso 5:15-16; Basi, muwe waangalifu jinsi mnavyoishi: Msiishi kama wapumbavu, bali kama wenye hekima. Tumieni vizuri muda mlio nao maana siku hizi ni mbaya.

***Yaweza kuwa Mungu alikuweka mahali ulipo kutumikia kusudi kuu kuliko unavyo fikiri.***

Esta aliogopa kwa kweli. Alikuwa ameenda- hakika- kutoka kwa nyumba ya umasikini hadi nyumba ya kifalme kwa sababu ya kibali cha Mungu juu ya maisha yake. Esta alikuwa mfungwa katika nchi ya kigeni na wakati neno lilisambaa kwamba mfalme alikuwa akimtafuta bibi harusi mpya, alichaguliwa kama mgombea. Hatimaye, alichaguliwa kuwa malkia mpya. Ni timizo la ndoto iliyoje! Alionekana alipangiwa kuwa pale. Kisha, mara tu maisha yalipo onekana mazuri sana shida ikatokea. Mpango wa kuangamiza taifa lake lote ukaanza na mfalme peke yake ndiye angeweza kuzuia. Kama malkia wake angeuliza usaidizi wake. Lakini sheria ya nchi ilitangaza ya kuwa alikuja bila kupewa idhini mbele ya mfalme na angeuwawa asingepata kibali kutoka kwa mfalme.

Esta aliogopa na hakujua cha kutenda. Aliuliza ushauri kutoka kwa mjomba wake. Alijua ya kwamba Mungu alikuwa na mpango juu ya watu wake na jukumu mpya ya Esta kama malkia ni mapenzi ya Mungu. Alimwambia kuwa hatima yake (Kama malkia) ilikuwa ni fursa ya kuhusika katika mpango wa Mungu. Umejiuliza jukumu lako maishani ni lipi? Yaweza kuwa Mungu amekuweka mahali ambapo ulipo kutumikia kusudi kuu kuliko unavyo fikiri? Muuliza akudhihirishie hatima yako ilivyo fursa ya kuhusika katika mpango Wake.

*<u>Ombi la leo</u>*

Baba, najua una mpango- sio tu wa dunia nzima ila wangu pia. Tafadhali nionyeshe jukumu langu na unipe ujasiri wa kuutekeleza. Njia zako ni kamilifu – ahsante kwa kuwa Baba mkuu.

*<u>Maandiko ya leo</u>*

Esta 4:14; kwa maana wewe ukinyamaza kabisa wakati huu ndipo kutakapowatokea Wayahudi msaada na wokovu kwa njia nyingine; ila wewe utaangamia pamoja na mlango wote wa baba yako; walakini ni nani ajuaye kama wewe hukuujia ufalme kwa ajili ya wakati kama huo?

## *KWA NINI sio ya umuhimu sana wakati NI NANI ni Mungu*

Katika Bibilia watu wengi waliambiwa na Mungu wafanye mambo kadhaa amabayo yalionekana kwa wakati huo, kukosa maana. Kwa mfano Namani, mwenye ukoma, aliambia ajitumbukize  mto Yorodani mara saba; Ezekieli aliambiwa anyoe kichwa chake; Mjane aliambiwa amtume mwanaye wa kiume aombe nyungu tupu kutoka kwa jirani; Yesu alifanya matope na akampaka macho ya yule kipofu, akimwambia

aende ajioshe; Paulo na Sila walianza kuimba wakiwa gerezani usiku wa manane,… mambo haya yote hayangeeleweka ilhali yote yalikuwa ni kwa mpango Mungu wakimuujiza kuhusu maisha yao.

*Kwa nini* sio muhimu sana tunapojua kuwa *ni nani* ni Mungu. Usiwekee Mungu viwango za hekima ya kidunia, mawazo ya kiutu ama kuelewa kwako binafsi. Wacha Mungu awe ni Mungu.

*Ombi la leo*

Bwana, kuna baadhi ya mambo naweza kosa kuelewa na wakati mwingine labda sitajua sababu unanifanya mimi niseme vile ninavyosema, ama nifanye ninavyofanya, hata hivyo na ungama kwamba nita kutii wakati wote na nitafuata neno Lako.

*Maandiko ya leo*

Zaburi 78:41; wakarudi nyuma wakamjaribu Mungu; wakampa mpaka mtakatifu wa Isiraeli.

Mathayo Mtakatifu 13:58; Kwa hiyo, hakutenda miujiza mingi pale kwa sababu ya kutoamini kwao.

1 Peter 5:7; Jiwekeeni hazina mbinguni ambako nondo na kutu hawawezi kuiharibu, wala wezi hawaingii wakaiba.

## ***Ni bure kuwa na nia bila mpango***

Ndoto na maono ni lugha ya Roho na kwa hayo Mungu hutia moyo kila mtu aliye na ukuu uliopita hali zao za sasa. Hata hivyo himizo la Mungu sio linalogharimika ili kutimiza kusudi Lake maishani mwako. Ili tufaulu, lazima tuwe na bidii sio tu kwa kusikia *ambacho* Mungu anataka kitendeke lakini *vile* anavyotaka kutimiza. Kisha, hatuna budi kutenda kazi ili tuone kusudi hilo likitimilika.

Nuhu alisikia Mungu akimwambia ajenge mashua. Hata hivyo bila maagizo ya Mungu kwa kujenga mashua na kufuatiliwa na jitihada ya Nuhu kwa muda wa miaka mia moja, safina halingelikuwepo. Mungu alimwambia Musa ajenge hekali na kisha akampa maagizo yenye kumakinika kwa kila hatua ya mradi. Kisha ikamchukua Musa na wana wa Isiraeli miezi mingi kuukamilisha mpango wa Mungu. Iweni na bidii ya kujua mapenzi  ya Mungu na kupata mpango wa Mungu. Kisha, tenda kazi ili uone ikitimia.

*Ombi la leo*

Mungu, ningependa kutimiza kusudi Lako maishani mwangu. Nipe mipango Yako na initunukie nguvu za kutenda kazi na kuona mapenzi Yako yakitimia.

*Maandiko ya leo;*

Mithali 21:5; mawazo ya wenye bidii huuelekea utajiri tu; bali kila mwenye pupa huuelekea uhitaji.

Mithali 13:4; nafsi ya mtu mvivu hutamani asipate kitu; bali nafsi ya mwenye bidii itanenepeshwa.

Mathayo Mtakatifu 9:38; Kwa hivyo mwombeni mwenye shamba atume wavunaji shambani mwake."

## ***Kwa nini utosheke na kuwa nahodha wakati amepangiwa kuwa mfalme.***

Ilifika wakati katika maisha ya Daudi ambapo alikuwa nahodha wa jeshi lote la Isiraeli. Alikuwa amefaulu katika jukumu hili hivi kwamba hata nyimbo zilitungwa kuhusu ushindi wake zikitangaza hakuna mwingine angeweza kufanana naye. Daudi, alizungukwa na watu waaminifu, waliomfuata pasipo maswali na walimuunga mkono kwa kwa uamuzi wake wote. Daudi angejiwazia kuwa katika siku yake kuu akifurahia ushindi wake na kutazamia kustaafu kwa umaarufu. Hata hivyo, Mungu alikuwa amemuita kufanya jambo kuu zaidi kuliko hili. Hatima hulazimu tusahau mambo hayo yaliyo nyuma na kuchuchumilia yale yaliyo bado mbele ili tuweze kufikia mwito wetu mkuu zaidi kwa Mungu kumpitia Kristo Yesu. Pengine uko katika kiwango cha fanaka ya sasa na kumbe Mungu amekutayarishia mambo makuu. Kwaweza kuwa na gharama ya kuondoka katika imani lakini itakugharimu nini usipo fanya hivyo?

*Ombi la leo*

Mpenzi Mungu, nisaidie kutototosheka na chache kuliko sadaka yangu kuu zaidi Kwako. Nipe neema ya kufikia mwito wangu wa juu na nifikia utendaji wangu mkuu zaidi kwa utumishi wa Ufalme Wako.

*Maandiko ya leo*

Wafilipi 3; 13-14; ndugu, sijidhanii nafsi yangu kwamba nimekwisha kushika; ila natenda neno moja tu; nikiyasahau yaliyo nyuma

nikiyachuchumilia yaliyo mbele; nakaza mwendo, niifikilie mende ya thawabu ya mwito mkuu wa Mungu katika Kristo Yesu.

2 Timotheo 4:7; Nimefanya bidii katika mashindano, nimemaliza safari yote na imani nimeitunza.

## ***Kizazi kionacho kurudi kwa Yesu kitakuwa ni kanisa lililo tayari kwa kurudi kwake.***

Tangu wakati wa Kristo, Wakristo wamekuwa wakisubiri kurudi Kwake. Kila kizazi cha waumini kwa miaka 2000 iliyopita kilitamani kumuona Yeye katika maisha yao. Yesu amekuwa akitazamia nini? Anatazamia kila kizazi kitaeneza ufalme Wake kwa njia ya kufanya wanafunzi wa mataifa yote na kutangaza injili Yake kwa mataifa yote ya dunia.

Kizazi chako kina kazi ya kufanya na kwa sasa inabaki kuwa haijakamilika. Yesu hatarudi hadi kazi ikamilike. Kizazi kitakacho muona Yesu kitakuwa ni kile kiko tayari kwa kurudi Kwake. Unaweza kufanya nini siku ya leo?

*Ombi la leo*

Baba, pea kizazi chetu ari ya yakuufikia ulimwengu na habari ya Kristo. Tupe uharaka na utusaidie tusikose fursa yoyote ya kueneza injili.

*Maandiko ya leo;*

Mathayo mtakatifu 28:19; Nendeni basi, mkawafanye watu wa mataifa yote wawe wanafunzi wangu; mkiwabatiza kwa jina la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu.

Ufunuo wa Yohana 21:2; Nikaona mji mtakatifu, Yerusalemu mpya, ukishuka kutoka kwa Mungu mbinguni. Ulikuwa umetayarishwa vizuri kama bibi arusi aliyepambwa tayari kukutana na mumewe.

Ufunuo wa Yohana 22:20; "Naam! Naja upesi." Amina. Na iwe hivyo! Njoo Bwana Yesu!

## ***Labda haitagarimu ujasiri na haima kuipata, lakini itagharimu tabia kihifadhi.***

Wewaza fanya chochote unaweka mawazo yako kufanya. Lolote ambalo ndilo lengo lako, waweza kulifikia ukiwa na nia iliyo sawa na shabaha ya kuiazimia. Lakini wakati watu wengi wanapofika pale walitaka kufika

maishani, wao huanza kufanya mambo yao ya muhimu zaidi yaponyoke; wanajaribiwa kuruhusu mambo yasiyo na muhimu yawaondoe katika njia; wakati mwingine hata wao huanza kuruhusu uadilifu wao na tabia zao kudidimia.

Mfalme Sauli alishuhudia haya katika maisha yake mwenyewe. Ufalme wake hakuenda mbali kwa sababu alikosa kuwa mtiifu na mwaminifu kwa amri za Mungu. Chochote unachotafuta maishani- kumbuka labda haitachukua ujasiri na haima pekee kuipata, lakini pia italazimika kuwa na tabia kuihifadhi. Mruhusu Mungu aangalia tabia yak oleo.

*Ombi la leo*

Bwana, nataka tabia Yake idhihirike maishani mwangu. Nisaidie kuwa mwaminifu hata kwa mambo madogo zaidi; nikiafikia malengo yangu, nisaidie kubaki mnyenyekevu na wa kutii amri zako. Tafadhali nionyeshe maeneo maishani mwangu yanayohitaji kubadilishwa. Ahsante, Baba kwa anjili ya huruma na neema Yako.

*Maandiko ya leo*

1 Samueli 13:13-14; 13 Naye Samweli akamwambia Sauli, Umefanya upumbavu; hukuishika amri ya Bwana, Mungu wako, aliyokuamuru; kwa maana Bwana angaliufanya ufalme wako kuwa imara juu ya Israeli milele. - Lakini sasa ufalme wako hautadumu; Bwana amejitafutia mtu aupendezaye moyo wake, naye Bwana amemwamuru yeye kuwa mkuu juu ya watu wake, kwa sababu wewe hukulishika neno lile Bwana alilokuamuru. -

1 Samueli 15:26;; kwa sababu umelikataa neno la Bwana, Bwana naye amekukataa wewe, usiwe mfalme wa Israeli.

## *Umasikini ni jambo la kimawazo sio hali ya maisha*

Kuishi katikati ya mawazo ya kiumasikini itakugharimu yote uliyo nayo, furaha yako, amani yako, wema wako, na thawabu yako ya umilele. Mawazo ya kiumasikini yaweza kutokana na mzizi wa uchoyo, uzembe ama, kukosa imani. Yaweza pia kutokana na laana ya vizazi vya jadi inayopitishwa kupitia jamii, utamaduni, ama hali za maisha. Mungu, hata hivyo, hana mawazo ya kiumasikini.

Maelezo ya mbinguni yanaeleza kuna mitaa ya dhahabu, lango za lulu, na nakshi ya mawe ya dhamana. Mapenzi ya Mungu kwa wanawe ni mawazo yanayo husu maisha ya utele, wakimwamini baba wao wa

mbinguni kwamba atawatwalia mahitaji yao yote, kulingana na utele wake sio kulingana na mahitaji yao. Mali ya mtu hulinganishwa na utele wa mambo anayo yamiliki. Vunja roho ya umasikini na uanze kushiriki kwa mpango wa Mungu kuhusu maisha yako.

*Ombi la leo*

Baba, nisaidie kujiona kama unionavyo Wewe na unibadilishe nifanyike kama Wewe unavyonihitaji kuwa. Vunja roho yeyote mbaya maishani mwangu na uniweke huru katika Jina la Yesu!

*Maandiko ya leo*

Luka Mtakatifu 12:15; Basi, akawaambia wote, "Jihadharini na kila aina ya tamaa; maana uzima wa mtu hautegemei wingi wa vitu alivyo navyo."

Mithali 10:15 Mali ya mtu tajiri ni mji wake wa nguvu; Uangamivu wa maskini ni umaskini wao

Mithali 20:13; usipende usingizi la sivyo utakuwa masikini, uwe macho nawe utakuwa na chakula cha akiba.

## *Umasikini ni jambo la mawazo: fukara ni hali ya maisha...zote mbili zaweza badilika*

Nimewajua watu na vitabu vimeandikwa kuhusu watu wanaomiliki mambo mengi ingawa wana imani kidogo. Maisha yao ya ilafi na yalio-jaa uwoga yamewateka nyara kuishi maisha ya huzuni, wakitafuta yote wawezayo bila kufurahia yote walio nayo wala kutumia pasipo manufaa yoyote. Na mali yao iliyo nyingi, hawa watu hufariki kama wamejaza umasikini.

Pia nimewajua watu waliokuwa masikini na walikuwa na kidogo sana cha uzuri wa ulimwengu huu kwa jina lao. Lakini, kwa nyakati zingine, hawa watu waliokuwa wamemiliki zaidi ya kile pesa zinaweza kununua. Upendo, furaha, amani, subira ni matunda ya Roho, sio ya mali. Hata hivyo, sio wale wenye umasikini ama wale fukara walio pangiwa kubaki jinsi walivyo sasa. Mabadiliko yako kwa kila mwanadamu na yanaweza kuanza katika maisha yako siku ya leo. Amini Mungu na kile ulicho nacho naYe atakupea zaidi. Anza leo kwa kupanda mbegu zako kwa mavuno ya siku za usoni.

*Ombi la leo*

Baba, naamua kukuamini Wewe kwa yote niliyo nayo. Nisaidie kusoma Neno Lako na nipate njia Yako ya ufanisi na unipe hekima kusaidia wengine njiani yangu.

*Maandiko ya leo*

Yakobo 2:5; Ndugu zangu wapenzi, sikilizeni! Mungu amechagua watu ambao ni maskini katika ulimwengu huu ili wapate kuwa matajiri katika imani na kupokea Utawala aliowaahidia wale wanaompenda.

Luka Mtakatifu 19:8; Lakini Zakayo akasimama akamwambia Yesu, "Sikiliza Bwana! Mimi nitawapa maskini nusu ya mali yangu, na kama nimenyang`anya mtu yeyote kitu, nitamrudishia mara nne."

Mithali 19:17; Amhurumiaye maskini humkopesha Bwana; Naye atamlipa kwa tendo lake jema.

## *Ni jambo la ujasiri kuenda kuwatafuta maadui wako. Lakini uhodari ndiyo utakaohitaji ukisah wapata.*

Zaidi ya inavyowezekana, umeisikia hadithi ya Daudi na Goliathi mara zisizohesabika. Kijana wa kuchunga aliamua kuwa atasimama kinyume na Mfilisti jitu aliyetisha jeshi la Isiraeli. Daudi alipojitoa mhanga kupigana na Goliathi, hakuna aliyeamini kuwa angeweza. Watu wengi hodari walikuwa wametafuta maadui wao wa Kifilisti hadi hapa, lakini ilipofika wapigane, hakuna aliyekuwa na ujasiri.

Ujasiri sio kukosa uoga ila ni kila watu hodari hufanya wakikumabana na uoga. Ujasiri wa Daudi ulikuwa ni zaidi ya maongeo duni. Machoni mwa huyu jitu, Daudi alitangaza imani yake na akashida vita. Ni mkubwa aliye ndani yako kuliko aliye ndani ya ulimwengu. Usiwache maadui wako wageuke kwako na kukumaliza. Kuwa na ujasiri na upigane nao kwa imani.

*Ombi la leo*

Bwana, ahsante, kwa maana Neno Lako linasema hautaniwacha wala kunitupilia mbali. Unatuambia tusiogope; nisaidie nitii Neno Lako, nijaze na ujasiri na imani kuwa hautaniwacha kamwe. Ahsante kwa kufanyike mwamba wangu na ngome langu.

*Maandiko ya leo*

Zaburi 121:1; Nitayainua macho yangu niitazame milima, Msaada wangu utatoka wapi? 2 Msaada wangu u katika Bwana, Aliyezifanya mbingu na nchi.

Isaya 12:2; Tazama, Mungu ndiye wokovu wangu; Nitatumaini wala sitaogopa; Maana Bwana YEHOVA ni nguvu zangu na wimbo wangu; Naye amekuwa wokovu wangu. -

Warumi 8:31Kutokana na hayo, tuseme nini zaidi? Ikiwa Mungu yuko upande wetu, nani awezaye kutupinga?

Warumi 8:37; Lakini, katika mambo haya yote, tumepata ushindi mkubwa kwa msaada wake yeye aliyetupenda.

## ***Kungonjea ni muhimu na mara nyingi hubainishwa na mambo zaidi ya yale tunaweza kusimamia.***

Manda moja Yesu alitumia mara nyingi kuelezea ujuzi wa ukristo ilikuwa kilimo. Aliongea kwa kanuni za kupanda mbegu, kuzaa matunda, na kuvuna mavuno. Kuna siri imefunikwa na kupanda mbegu na kuziona zikikua. Wakati wa kupanda na jinsi jua kinajigawa na maji lazima yawe kiwango sawa ili yalete mavuno. Twaweza kuendelea kufanya kazi, tuweke vifaa vya kazi vilivyo sawa, na tujue ni nini tunatafuta, lakini muujiza wa mbegu kuzaa matunda hauko kwa mikono yetu.

Wakati ni muhimu, na wakati hubainishwa sanasana na mambo yaliyo zaidi ya usimamizi wetu. Mkulima hawezi kubashiri wala kubainisha ni wakati upi jua litawaka wala mvua itaanguka, lakini aweza kuendelea kufanya kazi nakujitayarisha mavuno yanapokuja. Kwa njia iyo hiyo, kazi yetu sio kuelewa wakati wa Mungu, ila kuwa tayari wakati ukifika. Kumbuka, sio lazima uelewe jinsi Ufalme wa Mungu unavyofanya kazi ili uweze kuufanyia kazi.

*Ombi la leo*

Bwana, kunayo mambo mengi sana nisiyoweza kusimamia, lakini naamini wakati wako makamilifu kwa yote yanayoendelea maishani mwangu. Nisaidie nifanye kazi kwa bidii na niwe mwaminifu kwa majukumu yangu yote kwa sababu ninajua Utayafuata na mavuno mara ndufu.

*Maandiko ya leo*

Mariko Mtakatifu 4:26-29;. Yesu akaendelea kusema, "Ufalme wa Mungu ni kama ifuatavyo. Mtu hupanda mbegu shambani.Usiku hulala, mchana yu macho na wakati huo mbegu zinaota na kukua; yeye hajui inavyofanyika. Udongo wenyewe huiwezesha mimea kukua na kuzaa matunda: kwanza huchipua jani changa, kisha suke, na mwishowe nafaka ndani ya suke. Nafaka inapoiva, huyo mtu huanza kutumia mundu wake, maana wakati wa mavuno umefika."

2 Timotheo 4:2; hubiri huo ujumbe, sisitiza kuutangaza (iwe ni wakati wa kufaa au wakati usiofaa), karipia, onya na himiza watu ukiwafundisha kwa uvumilivu wote.

1 Petro 3:15; Lakini mtukuzeni Kristo kama Bwana mioyoni mwenu. Muwe tayari kumjibu yeyote atakayewaulizeni juu ya matumaini yaliyo ndani yenu,

## *Usoni mpya ukizaliwa utamaliza ukale*

Dhamana ya siku zetu za usoni kwa ukweli ni kwamba unaweza kubashirika kulingana na mipango na uamuzi tufanyao siku ya leo. Wakati mwingine tunaendeshwa na kuhimizika lakini mambo yetu ya dhamana yanakuwa na makosa. Mtume Paulo alipokuwa akiitwa Saulo, alikuwa ni tishio kwa kanisa la awali. Kwenye barabara ya Dameseki alipata mkutano na Mungu wa kubadilisha maisha yake. Kwa muda wa siku tu, Mungu akamchukua kutoka kwa tishio la kuchinja akipumua uasi kinyume na Mungu na watu Wake hadi akafanyika mhubiri aliyejazwa na Roho Mtakatifu. Matendo ya Mitume sura ya tisa inasema kwamba hapo na hapo Paulo akahubiri Kristo, kwamba yeye ni Mwana wa Mungu aishiye.

Kuzaliwa kwa usoni mpya kutaweka kikomo kwa mambo ya kale. Lengo la Paulo lilikuwa ni kumjua Kristo, kufanana na Kristo, na kuwa chote ambacho Kristo alikuwa amepanga kwa anjili yake.paulo alisema hili, “jambo majo mimi nafanya, nasahau mambo hayo yaliyo nyuma yangu, nakuchuchumilia hayo mambo yaliyoko mbele yangu” huu ni mfano mzuri kwetu sote kufuata. Tusiishi kwa mambo ya kale. Badala yake tukue katika ufahamu wa Mungu kwa kutia maanani husiano wako na Yeye sasa. Jua kwamba amesha samehewa, kisha enenda kwa maisha ya imani na utiifu. Tazamia maisha ya maana zaidi kwa sababu ya tumaini lako ndani ya Kristo.

*Ombi la leo*

Baba, ahsante kwa neema Yako ya wokovu. Kupitia damu ya Yesu niko huru kutokana na siku zangu za kale. Najiachilia Kwako leo, kukujua zaidi, kuwa kama Wewe zaidi, na kuishi maisha yangu kulingana na mappenzi Yako.

*Maandiko la leo*

2 Wakorintho 5:7Mtu yeyote akiungana na Kristo huwa kiumbe kipya, mambo ya kale yamepita, hali mpya imefika.

## ***Ni Nadra sana mtu afe kwa anjili ya jambo ambalo hakutaka kuishi kwa sababu yake***

Yohana Mbatizaji alisema kwamba alibatiza na maji lakini Masihi akija atabatiza na Roho Mtakatifu na moto. Katika Luka 24, Yesu aliwaambia wanafunzi Wake wangonjee Yerusalemu hadi wavishwa na nguvu kutoka juu mbinguni. Matendo ya Mitume 1:8, inaendelea kwa kusema, kwamba yeyote aliyepokea nguvu za Huyu Roho Mtakatifu atapewa uwezo wa kufanyika shahidi. Neno shahindi katika Matendo Ya Mitume 1:8 inamaanisha kuwa anayekufa kwa anjili ya jambo.

Anayekufa kwa anjili ya jambo sio kuhusu kukufa kiasili pekee lakini katika nakala hii inaeleweka kama kumaanisha, kuishi maisha yako kama umeachilia mambo yote mengine na kufuata mapenzi ya Mungu peke yake. Kama Mtume Paulo alivyosema, ‘ kuishi ni Kristo, na kufa ni faida.’ Waumini wengi hujiwazia wakiwa wamejitolea kukufa kwa anjili ya Kristo. Hata hivyo, ni nadra mtu atakufa kwa anjili ya kitu ambacho hayuko tayari kukiishia.

*Ombi la leo*

Baba, nakupa Wewe maisha yangu ninapoishi. Naamua kuishi maisha yangu nikijiachilia kwa mpango Wako na kufanyika shahidi Wako katika hali zangu zote za maisha. Nipe neema Yako Bwana, katika jina la Yesu, Amina.

*Maandiko la leo*

Wagalatia 2:20; na sasa naishi, lakini si mimi tena, bali Kristo anaishi ndani yangu. Maisha haya ninayoishi sasa naishi kwa imani, imani katika Mwana wa Mungu aliyenipenda hata akayatoa maisha yake kwa ajili yangu.

Wakolosai 3:1-3; Basi, ikiwa mmefufuka pamoja na Kristo, panieni mambo ya juu, kule Kristo aliko, ameketi upande wa kulia wa Mungu.

Muwe na hamu ya mambo ya huko juu, na siyo mambo ya hapa duniani. Maana ninyi mmekufa na uzima wenu umefichwa pamoja na Kristo katika Mungu.

## ***Kama hakuna chochote katika maisha yako ambacho waweza toa kwa anjili ya maisha yako, basi kwa kuhuzunisha wewe ndiwe kila kitu cha dhamana zaidi unachojua.***

Rahabu alikuwa ni kahaba kutoka Kanani aliyemalizia kwa kufanyika markia wa Yuda na mama wa Boazi. Ruthu alikuwa mjane wa Moabi na pia mtu wa kuomba omba aliyemalizia kwa kumuoa Boazi na kufanyika mama wa Obedi. Laeh alikuwa bibi arusi ambaye hakuwa napendeza na mke asiyependwa na Yakobo aliyemalizia kwa kuwa mama wa Yuda. Hawa wa mama wote pamoja na wengine wengi hawakuanzia maisha vizuri na hata ingawa walipitia kwa shida nyingi kwa njia yao, walimalizia kwa nakala ya wazazi wa nyanya ya Yesu.

Tunapoanzia safari sio pa muhimu kama pale tunamalizia. Labda kwa wakati huu maishani mwakounapata kidogo kuliko mawazo yako kuhusu maisha. Labda hali na matukio yaliozidi uwezo wako yanaonekana kama yamekufunga wewe kwa maisha madogo kuliko vile unavyotamani. Usife moyo, Mungu hajakusahau wewe ba ako ba mpango wa kukupeleka kwa siku yako kuu. Mwamini Yeye na umwache akuwe kielelezo chako.

*<u>Ombi la leo</u>*

Mpenzi baba, tafadhali nipe hekima na neema kuvumilia utaratibu wa maisha, nikijua itanielekeza kwa siku zangu na kwa ubora wangu na tumaini.

*<u>Maandiko la leo</u>*

Yeremiah 29:11 kwa kuwa na jua mawazo ninayowaza kukuhusu, asema Bwana, mawazo ya amani na sio ya ubaya, kukupa tumaini na siku bora za usoni.

2 Wakorinitho 4:17-18; Taabu tunayopata ni kidogo, tena ya muda tu: lakini itatupatia utukufu upitao matazamio yote, utukufu ambao hauna mwisho. Hivyo tunatazamia kwa makini si vitu vinavyoonekana, bali

visivyoonekana. Maana vinavyoonekana ni vya muda tu; lakini vile viSivyo onekana ni vya milele.

## *Niamini Mimi, Mungu akisema umekosea, umekosea!*

Wakati mwingi watu wakifikiria wamekosea, watabadilisha mawazo yao kwa sababu kila mtu anapenda kuwa sawa. Tunajaribu kusahihisha tunachowazia, tunachotaka, na tunachihisi katika hali na na shani mambo ambayo tunakabiliana nayo na wakati mwingi twaweza kujiona kuwa sahihi tukitazama kwa mtazamo wetu wenyewe. Kwa mfano kama mtu amekuumiza kwa undani, amekusaliti, ama kukunena kwa ubaya mambo yasiyokuwa ya ukweli, waweza hisi kama uko saw kwa kutomsamehea mtu kama huyu.

Hata ingawa unafahamu Neno la Mungu linatuhimiza tusamehe. Hivyo ndivyo ilivyo kwa maagizo mengine Mungu anayotupea kutoka kwa Neno Lake: amri kama ya kunyenyekea, kutii, kupendana, usiseme uongo na zingine nyingi. Bila kujalisha unahisi vipi anavyohisi, ama ni kwa nini waweza kuhisi unavyohisi, Mungu akisema umekosea, umekosea… na nimakosa kutotii Mungu.

*Ombi la leo*

Bwana, natoa yote yangu Kwako na kwa huruma Zako. Ni dhihirishie mimi eneo lolote maishani mwangu ambalo lina makosa mbele Zako. Naungama dhambi zangu. Zifunike kwa damu Yako na ufanye roho na mikono ya kuwa safi katika Utakatifu Wako.

*Andiko la leo*

Zaburi 43:3 tume nuru Yako na ukweli Wako: wacha ziniongoze mimi; wacha zinielekeza kwa mlima Wako Mtakatifu, na kwa nyumba Yako. Kisha nitaenda kwa madhabahu ya Mungu; kwa Mungu furaha yangu tele: ndiyo, na kunumbi nitakusifu Wewe, ewe Mungu, Mungu wangu.

## *Mwito ndiyo fursa Mungu atupeayo, ilhali neema ni uwezo anaotukopesha ili tuchukua fursa hiyo.*

Mungu alikuwa amshasikia vilio vya watu wake waliokuwa wametekwa nyara Misri, na alikuwa na mpango kuhusu ukombozi wao. Kwa njia Yake na wakati Wake Yeye, akapanga Musa aanze safari kuelekea Misri na aambia Farao aachilie wana wa Isiraeli. Hadithi hii imenjaa matukio ya miujiza- kutokea kwa mapigo hadi kwa bahari ya shamu kufanya

njia. Mungu angewaachilia watu Wake kutoka kwa mkono wa Farao akiwa peke Yake, lakini akachagua kuwacha mtu duni kufanya jukumu kubwa katika utaratibu huu. Mungu alikuwa na mpango; Musa alikuwa na fursa ya kuhusika.

Lakini Musa kwa mara ya kwanza hakuwa na uhakika, na dhiitisho lakini Mungu akamhakikishia ya kwamba atampatia chochote alichihhitaji kuendeleza huduma. Mwito ni fursa Mungu anatupa, ilhali neema ni uwezo ana bado hauna dhibitisho? Unaweza kuwa na imani ya kwamba Yeye atakupatia neema inayotakikana kumaliza jukumu!

*Ombi la leo*

Bwana, ahasante kwa kutuhusisha katika mipango Yako. Tafadhali nikumbushe ya kwamba kila wakati uko nami, na mimi ni mwaminifu. Unanipatia uwezo ninaohitaji kufaulu. Kweli naweza kufanya mambo yote kupitia Kristo anayenipea Nguvu.

*Maandiko ya leo*

Kutoka 4:11; bwana akamwambia, " ni nani aliyekifanya kinywa cha mwanadamu, au ni nani afanyaye mtu kuwa bubu au kiziwi au mwenye kuona, au kuwa kipofu? Si mimi, BWANA? Basi sasa enenda nami nitakuwa pamoja na kinywa chako, na kukufundisha utakalolinena.

Wafilipi 4:13; nayaweza mambo yote katika yeye anitiaye nguvu.

## *Aidha tunajenga madaraja, tunainua vizuizi, ama kuimarisha viwanja vya vita na wengine*

Hivi punde ama hapo awali tunaposafiri katika barabara ya maisha tutakumbana na majanga katika uusiano wetu na wengine. Inaweza kuwa ni mume ama mke ambaye ameamua kwenda njia tofauti, rafiki ambaye ametuingilia kati, ama mshiriki wa kikazi ambaye kwa ghafla amesimamisha ahadi zake.Tusipuuze ya kwamba, huenda ikawa sisi wenyewe tuligeuka vibaya wakati Fulani katika njia yetu.

Tufanye nini wakati kama huo maishani?  Tunafaa kuchunguza uhusiano huo na hali kulingana na nuru ya Neno la Mungu. Tunapofuata ramani Yake ya barabarani, tutaona bila kizuizi shinikizo la msamaha likituelekeza, huruma ikituita, na neema ikitushika mkono. Kumbuka katika kila hali labda tunajenga madaranja, tunainua vizuizi, ama kuimarisha viwanja vya vita na wengine… mara nyingi huu ni uamuzi wetu.

*Ombi la leo*

Baba, nisaidie siku ya leo kufuata mpango Wako na njia katika kila kitu, hata uhusiano wangu na watu wengine. Nisaidie mahali nichukua mgeuko mbaya na unipe neema na nguvu kupeana msamaha uo huo kwa wengine ninaposafiri kwa maisha siku ya leo.

*Maandiko ya leo*

Wagalatia 6:1 Ndugu, kama mkimwona mtu fulani amekosea, basi, ninyi mnaoongozwa na Roho mwonyeni mtu huyo ajirekebishe; lakini fanyeni hivyo kwa upole, mkiwa na tahadhari msije nanyi wenyewe mkajaribiwa.

2 Wakorinitho 5:18Yote ni kazi ya Mungu mwenye kutupatanisha sisi naye kwa njia ya Kristo, akatupa nasi jukumu la kuwapatanisha watu naye.

## ***Tunapohubiri kuhusu dhambi ni vizuri tuwe na mtazamo kuwa hawakukusudia kutenda.***

Mojawapo ya picha kuu za msamaha ndani ya Bibilia ni ile ya mama aliykutwa kwa uzinzi na akaletwa kwa Yesu ili ahukumiwe. Waliomuleta mbele za Yesu walitishika kwa majibu Yake ya huruma kwa mama huyu na jinsi alitumia fursa hii kuwaonyesha makosa yao na dhambi zao wenyewe. Funzo Lake lilikuwa na sura mbili: huruma ni kuu kuliko hukumu, na kama sio kwa neema ya Mungu, hapo naenda mimi.

Muda mchache baadaye, Yesu alimalizia ujumbe Wake wa msamaha na neema alipokuwa akininginia msalabani Kalivari. Alikufa kwa sababu ya huyo mwanamke wa uzinzi na kwa anjili ya wale waliomsulubisha na kwa mimi na wewe. Maneno Yake bado yanapiga kengele enzi zote… “ wasamehe Baba, maana hawajui wanalo litenda.” Tunapoendeleza ujumbe wa injili, tufanye hivyo kwa mtazamo kama vile Yesu alivyojionyesha msalabani. Tunapohubiri dhambi, tuwe wa rehema na tutazame ni kama hawa kumaanisha kufanya.

*Ombi la leo*

Baba, ahsante kwa kunisamehe mimi kila wakati na kuniwazia mema. Nisaidie kuangaza mtazamo huo wa neema kwa wengine leo ili nao pia, waje katika ufahamu wa upendo Wako

*Maandiko ya leo*

Luka Mtakatifu 23:34Yesu akasema, "Baba, uwasamehe kwa maana hawajui wanalofanya." Kisha wakagawana mavazi yake kwa kuyapigia kura.

Mathayo Mtakatifu 7:1"Msiwahukumu wengine, msije nanyi mkahukumiwa na Mungu;